TANGAZO LA SERIKALI NA. 555 la tarehe 26/7/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (1)(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SUMBAWANGA (“SUMBAWANGA WSSA”), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Jina la Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri hii Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga (“Sumbawanga WSSA”), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachuliwa imeanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya Bei

3.Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Sumbawanga WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 30 Septemba 2019 au kabla, Sumbawanga WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Sumbawanga WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(c) Sumbawanga WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(d) Sumbawanga WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu

cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(e) Sumbawanga WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Sumbawanga WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Sumbawanga WSSA katika siku zijazo;

Kufuta Tangazo la Serikali.Na. 443 la 2017

5. Amri hii ya bei inafuta Amri ya Bei ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga Na. 2017-006.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba (a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi ($m^3$) | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 0-5 | 800 | 1,000 | 1,000 | 1,030 |
| | >5 | 975 | 1,010 | 1,130 | 1,250 |
| | >5-<20 | 975 | | | |
| Taasisi | 0-5 | 1,000 | 1,040 | 1,160 | 1,280 |
| | >5-<20 | 1,155 | | | |
| | >20 | 1,345 | | | |
| Biashara | 0-5 | 1,000 | 1,040 | 1,160 | 1,280 |
| | >5-<20 | 1,075 | | | |
| | >20 | 1,250 | | | |
| Viwanda | 0-5 | 1,155 | 1,200 | 1,340 | 1,480 |
| | >5-<20 | 1,250 | | | |
| | >20 | 1,440 | | | |
| Magari | 20 litres | 20 | 20 | 20 | 20 |

Jedwali Namba (b): Ada yaSasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maungansho kama Ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013. | Asilimia 20 ya Gharama za Maungansho kama Ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013. | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

Jedwali Namba (c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 30,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 30,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 30,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

Jedwali Namba (d): Tozo ya Sasa na Iliyodhinishwa ya Kuondoa Majitaka kwa Kutumia Gari ya Sumbawanga WSSA (Shilingi)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 57,000 | 60,000 | 63,000 | 66,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Taasisi | 69,000 | 73,000 | 77,000 | 80,000 |
| Biashara | 69,000 | 73,000 | 77,000 | 80,000 |
| Viwanda | 69,000 | 73,000 | 77,000 | 80,000 |

Jedwali Namba (d): Tozo ya Sasa na Iliyodhinishwa ya Kumwaga Majitaka katika Mabwawa ya Sumbawanga WSSA (Shilingi kwa Gari)

| Aina ya Gari | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Gari zenye uzito wa Tani3hadi5 | 7,000 | 8,000 | 11,000 | 16,000 |
| Gari zenye uzito wa Tani 7 | 10,000 | 11,000 | 16,000 | 21,000 |
| Gari zenye uzito waTani 10 | 20,000 | 21,000 | 27,000 | 32,000 |

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | 2019/2020 (Sh.) | 2020/2021 (Sh.) | 2021/2022 (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Dira za maji | 421,470,200 | 442,707,160 | 467,861,810 |
| Mabomba na viungio | 296,000,000 | 285,000,000 | 604,000,000 |
| Matangi ya maji | 80,000,000 | 70,000,000 | 60,000,000 |
| Majengo na Uzio | 1,436,032,630 | 790,000,001 | 470,000,000 |
| Bwawa la maji safi na miundombinu ya kutibu majitaka | 120,000,000 | - | - |
| VitendeakazizaKarakana | 80,000,000 | 90,000,000 | - |
| Mitambo | - | 282,032,630 | 500,000,000 |
| Pampu | 80,000,000 | - | 80,000,000 |
| Vifaavyaumeme | 90,000,000 | - | 118,032,630 |
| Magarinapikipiki | 166,000,000 | 91,000,000 | 16,000,000 |
| Komputanavifaavyake | 9,500,000 | 17,500,000 | 10,000,000 |
| Jumla | 2,779,002,830 | 2,068,239,791 | 2,325,894,440 |

*GN. NO. 555 (Contd.)*

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

| Maelezo | Kipimo | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Idadi y awateja wapya wa majisafi | Na | 515 | 565 | 616 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 25 | 25 | 25 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 95 |

JEDWALI LA NNE
MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| GHARAMA | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| Uzalishaji wa Maji | 679,997,847 | 809,616,588 | 849,620,459 |
| Usambazaji wa Maji | 27,875,979 | 29,269,778 | 30,733,267 |
| Matengenezo | 70,000,000 | 103,000,000 | 106,000,000 |
| Watumishi | 720,892,909 | 895,106,407 | 960,109,950 |
| Utawala | 322,103,921 | 337,969,118 | 354,627,575 |
| Matangazo | 13,493,764 | 14,168,452 | 14,876,875 |
| Matukio | 9,845,325 | 10,337,591 | 10,854,471 |
| Gharamaza Benki | 1,923,173 | 107,127,666 | 69,712,035 |
| Jumla (UendeshajinaMatengenezo) | 1,846,132,918 | 2,306,595,601 | 2,396,534,632 |
| Uchakavu | 556,843,444 | 677,092,423 | 803,831,867 |
| Uwekezaji | 463,492,736 | 631,570,435 | 808,442,430 |
| JumlayaGharamaZote | 2,866,469,098 | 3,615,258,459 | 4,008,808,929 |

Dodoma,
……………………………, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi mkuu*